JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram **"AFYA", DODOMA**
Nambari ya Simu: **+255 026 – 2323267**
E- Mail Na. ps@afya.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L. P 743,
**40478 DODOMA.**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AJIRA MPYA ZA MADAKTARI 1000

**Dar es Salaam, 16/5/2020**

Serikali katika juhudi zake za kutatua changamoto ya Rasilimali watu katika Sekta ya Afya imeajiri Madaktari Wapya 1000. Ajira hizi zilitolewa tarehe 20 Machi, 2020 na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akizungumza na Madaktari pamoja na watumishi wa Sekta ya Afya. Ajira hizi za madaktari 1000 zitapunguza changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya afya toka asilimia 65 ya upungufu uliopo sasa hadi kufikia asilimia 57.

Lengo la ajira hizi ni kuhakikisha tunapata Madaktari katika Mikoa ya pembezoni kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa zenye upungufu mkubwa wa watumishi wa afya.

Hivyo, Wizara inatoa rai kwa wale wote waliobahatika kupata ajira hizo kuripoti mara moja katika vituo vyao vya kazi walivyopangiwa. Aidha, inawaomba Waajiriwa wapya wote waweke uzalendo mbele ili kuokoa maisha ya Watanzania ambao wapo Mjini na Vijijini; na wote wanaohitaji kupatiwa huduma bora za Afya. Pia, wizara inawapongeza Wataalamu wote wa Sekta ya Afya nchini kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya katika mapambano dhidi ya Janga hili la kimataifa la COVID-19.

Madaktari hawa 1000 kati yao 610 ajira zao zimepangwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (**TAMISEMI**). Vilevile, madaktari 390 ajira zao zitasimamiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Orodha ya majina na vituo walivyopangiwa inapatikana kwenye tovuti ya Wizara **www.moh.go.tz**.

Imetolewa na:

Catherine Sungura
**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**IDARA KUU AFYA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi ya Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI)- (Wamepelekwa Zahanati kwenye Vituo vya kutolea huduma za Afya) | - | 610 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Amana | - | 7 |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Bukoba | - | 11 |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma | - | 7 |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita | - | 34 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa | - | 7 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi | - | 12 |
| 8 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kitete, Tabora | - | 11 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ligula, Mtwara | - | 11 |
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara | - | 10 |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara | | 23 |
| 12 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Maweni, Kigoma | - | 13 |
| 13 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mawenzi, Moshi | - | 3 |
| 14 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | - | 7 |
| 15 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro | - | 7 |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mt. Meru, Arusha | - | 7 |
| 17 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwananyamala | - | 6 |
| 18 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe | - | 13 |
| 19 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Sekou Toure, Mwanza | - | 7 |
| 20 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga | - | 13 |
| 21 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu | - | 11 |
| 22 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida | - | 11 |
| 23 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Sokoine, Lindi | - | 5 |
| 24 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea | - | 11 |
| 25 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | - | 14 |
| 26 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Sumbawanga | - | 11 |
| 27 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga | - | 12 |
| 28 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke | - | 4 |
| 29 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tumbi, Kibaha | - | 3 |
| 30 | Vyuo vya Mafunzo ya Afya vya Wizara | - | 15 |
| 31 | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, (MNH) | - | 40 |
| 32 | Hospitali ya Benjamin Mkapa,(BMH) | - | 20 |
| 33 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili ,(MOI) | - | 10 |
| 34 | Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete,(JKCI) | - | 7 |
| 35 | Taasisi ya Saratani Ocean Road,(ORCI) | - | 7 |
| | **JUMLA** | | **1000** |